# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

…Kwa Neno Lako…

Lima, Peru
5-28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 13, Disemba 2018

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma



www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org


Mhariri

## Twendeni kwa furaha Betlehem…

Njia inayoelekea kwa Kristo mtoto, anayezaliwa masikini katika hori ya kulishia wanyama, ni ishara ya udhaifu wa kila mwanamume na mwanamke. Ni swala la kuifuata, kufurahia kufuata kwa makini fursa na zawadi ya huyo mtoto anayekusudia kamwe kutompoteza mtu yeyote, licha ya kuwa mtoto mchanga tu. Lakini labda tunasahau kwamba watoto wadogo watacheza kwenye shimo la fira, na ng'ombe na punda watatembea pamoja – ili kusema pamoja na nabii -.

Ni safari tunayoitwa kuifanya kila siku, tukifuata njia ya msingi. Namna ya kufanya pamoja na vijana wanaoalikwa kutokata tamaa hasa mbele ya shida za siku zijazo na wale ambao wamepoteza furaha ya kuishi na kufanya hivyo tu, wakizifanya siku zao zipite mara nyingi kuelekea kwenye usahaulifu.



Kutoka kwenye hori la kulia wanyama linazaliwa tumaini, ili kuamini katika Kanisa moja ambalo halibaki limesimama kumtafakari mtoto, bali kama wachungaji linarudi kutoka pangoni ili kutangaza kuwa ulimwengu haupaswi kuwa ghala kubwa la kuwekea silaha na zana lililowazi juu, kwamba masikini hawawi mabaki au kutumiwa kama chombo cha kupambia au kwa ajili ya kupiga kura za uchaguzi. Kile "kidogo" katika mikono ya mwanamke mwenye ujasiri na mwenye chachu hutualika kuondokana na ubinafsi, matokeo ya jamii ya utandawazi na ya kutojali, kuwa na uwezo wa kukataa hali ya utumwa, kutokataa kila aina ya mapokezi na kuendelea kutembea ili kutoacha kila kitu kuwa mikononi mwa wachache, iwe katika ngazi ya kiuchumi ama kisiasa. Ni njia isiyokubali mantiki ya vitu haramu na inakusudia kuonyesha mageuzi kwa ajili ya maisha ya kila mtu.

Twende kwa furaha Bethlehemu, lakini tukumbuke kurudi kutoka Bethlehemu ili kuwakumbusha tena wote kwamba hakuna mtoto aliyezaliwa hata mmoja anayezidi, lakini, mnisamehe, ana uso sawa na Kristo wa horini.

***Sr. Mimma Scalera, ASC***

## Muhtasari


*Mhariri*
- Twendeni kwa furaha Betlehem… 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- Kikosi kipya cha CIS 2

*Toka Ulimwengu ASC*
- Miaka 150 ya Uinjilishaji Tanzania 3
- Miaka thelathini tangu afariki Mtumishi wa Mungu Serafina 4
- Ubunifu 5
- Wakati watakatifu wakisongo mbele 6
- Kipindi cha ujana: huangaza utimilifu wa imani 7

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- "Chukia kosa na sio mkosaji" 8

*Ndani ya Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 9
- Sikukuu za kuzaliwa: Tunasherehekea maisha 9
- Waliorudi Nyumbani kwa Baba 9

# Kikosi kipya cha CIS

Wanakikosi kipya cha CIS, sr. Barbara Perali (Italia), sr. Elisabeth Mueller (Schaan), sr. Rani Padayattil (India) na sr. Toni Longo (USA) walikutana Roma kuanzia tarehe 9 hadi 18 Oktoba kwa ajili ya sala, majiundo ya kikundi, kuingia kwenye utume mpya na kwa ajili ya mpango wa miaka sita, tumefanya hatua nyingi pamoja... na tuko tu mwanzoni!

Kwenye jioni ya tarehe 9 Oktoba kikosi kilitambulishwa kwenye jumuiya mahalia ya Nyumba Kuu, ambapo kilipokea baraka kwa ajili ya kazi ambayo wataifanya pamoja. Siku tatu za kwanza zilitengwa kwa ajili ya sala, mashirikisho ya imani na hija huko Vallecorsa na Acuto. Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika, Sr. Dani Brought na Sr. Matjia Pavic, washauri wakuu wanaohusika na CIS, waliongoza na kuwezesha siku hizi.

Siku zilizofuata zilikuwa za kazi nyingi na kazi imezaa matunda yake ya kwanza: Ndoto ya CIS, mpango kwa ajili ya miaka sita na mpango dhahiri wa mwaka wa kwanza, halafu kazi yote ilikabidhiwa kwa Uongozi Mkuu. Tunaamini kuwa utume wetu utakuwa msaada kwa Uongozi Mkuu na kwa Shirika katika jitihada za "kumwilisha tasaufi/roho na karama ASC kwa mioyo inayotetemeka katika maduara ya ushirika yanayopanuka daima..." (kauli mbiu ya ndoto).

Wakati mtakaposoma nakala hii, tutakuwa tayari tumewasilisha mpango kwa Halmashauri Kuu Iliyopanuka, itakayokuwa imeandaliwa na kuunganishwa na liturjia wakati wa mkutano huu.

Tunawaalika kutembelea tovuti yetu ya Facebook ambapo mtapata baadhi ya picha na video mbili kwa kiitaliano na nyingine kwa kiingereza, ambapo tunajitambulisha na kuwaonyesha mahali tunapofanya kazi pamoja kwa ajili ya Shirika na ulimwengu wetu. Tunawaomba mtusindikize kwa sala zenu ili tuweze kufanya kazi kulingana na moyo wa Maria De Mattias.

***Kikosi CIS***








Centro Internazionale di Spiritualità

# Miaka 150 ya Uinjilishaji Tanzania


Mapandre wakiwa kwenye maandamano kabla ya ashimisho la Misa Takatifu


Maaskofu wakiwa kwenye maandamano kabla ya ashimisho la Misa Takatifu


Kanisa la Bagamoyo

Mnamo tarehe 4/11/2018 Kanisa Katoliki Tanzania Bara liliadhimisha Miaka 150 tangu Ukristo Ukatoliki uingie Tanzania bara kupitia Mji mkongwe wa Bagamoyo, na pia liliadhimisha miaka 100 toka Kanisa Katoliki la Tanzania Bara kupata Padre wa Kwanza Mzalendo (Mtanzania). Kilele cha adhimisho hili kilitanguliwa na siku tatu za maandalizi mbalimbali ya kiroho.

Uinjilishaji ulianzia Zanziba kabla ya kufika Tanzania Bara. Waliofika kwa mara ya kwanza ni mapadre wa Shirika la Roho Mtakatifu. Mwaka 1860 Akofu Moupoint ambaye Shirika la Roho Mtakatifu lilikuwa chini yake, alimtuma padre Amand Fava kuanzisha misioni Zanzibar. Wakati huo Zanzibar ilikuwa kituo kikubwa cha biashara ya utumwa. Takribani watumwa 60.000 waliuzwa hapo kila mwaka. Mwaka 1863 walitumwa mapadre wengine wawili wa Shirika la Roho Mtakatifu Padre Antonie Horner na Padre Etienne Baur na Mabruda wawili, Celestine na Felician. Mapadre na mabruda wa shirika la Roh Mtakatifu walisaidiana na masista wa mabinti wa Maria kutoka Reunion, wengi wao wakiwa watumwa waliokombolewa.

Misioni ya kwanza iliyoanzishwa Zanzibar tangu mwaka 1860 ilizaa matunda kidogo, kazi ya uinjilishaji ilikuwa ngumu, hata hivyo makao makuu ya misioni yalibaki huko, lakini shughuli nyingi zilihamishiwa Bagamoyo mwaka 1868. Misioni ya Bagamoyo ilianza tarehe 4 Machi 1868. Kazi ya kwanza hapo Bagamoyo ilikuwa ni ya kuwahudumia watumwa waliokombolewa. Hii kazi ilifanyika vizuri na wakawa na kijiji cha Wakristo, shule za kuwalea watoto na kufundisha kazi za ufundi kwa watu wazima. Sultani Seyyid Majid wa Zanzibar ambaye mwanzoni mwa misioni ndiye aliyekuwa mtawala wa Bagamoyo aliwasaidia sana wamisionari hao na alikuwa rafiki yao.

Wamisionari wa Bagamoyo walianza polepole kutembelea seheumu nyingine wakijifunza juu ya makabila mbalimbali na desturi zao wakiwa na lengo la kutafuta mahali pa kufungua misioni mpya.

Mwaka 1904 tayari walikuwa wameshafungua misioni 19. Leo kuna majimbo 34 Tanzania, mashirika mengi sana ya kitawa na idadi kubwa ya waumini wakatoliki. Itakumbukwa kwamba, Bagamoyo ni chimbuko la Ukristo Afrika Mashariki. Wamisionari hawa hawakubaki tu Tanganyika (Tanzania Bara), bali pia waliingia Kenya na sehemu zingiene za Afrika mashariki. Kwa hii historia fupi, Bagamoyo imekuja kuwa ni Mama wa Makanisa Katoliki siyo tu kwa Tanzania bali kwa Afrika ya Mashariki.

Maadhimisho haya nia yake ilikuwa ni kumshukuru Mungu kwa zawadi ya ukombozi na habari Njema iliyoletwa na wamisionari wa kwanza. Kumshukuru kwa zawadi ya mafanikio ambayo kanisa limeyapata kwa muda huu wote tangu wamisionari wa kwanza wafike hapa kwetu. Ilikuwa ni kutazama tulikotoka, tuliko na tunakoelekea. Kujikabidhi mikononi mwa Mungu ili kupitia kwetu, tunu hii ya imani tuliyoipokea tuendelee kuirithisha kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Ni kukumbuka na kukumbatia utume wa wamisionari wa kwanza hapa Tanzania bara, mateso yao, kujitoleo kwao na kufa wakiwa vijana wadogo kabisa, na jinsi walivyotoa maisha yao kwa ajili ya kutangaza Habari Njema ya Kristo Afrika ya Mashariki.

Bwana aendelee kulibariki Kanisa letu, nchi yetu na kuleta matunda mengi ya uinjilishaji.

***Wanovisi Maria A. Chanzi na Rosina R. Miro-kazi***


Masista ASC na wanovisi wawili walioshiriki siku mbili za maandalizi na sikukuu ya miaka 150 ya Uinjilishaji Tanzania Bara


Watu wazima na watoto wakati wa Misa

Eneo la Bara: Amerika
Region Brazil

# Miaka thelathini tangu afariki mtumishi wa Mungu Serafina



Kuanzia Oktoba 18 hadi 21 mwaka huu huko Altamira, iliadhimishwa miaka 30 tangu afariki Mtumishi wa Mungu SERAFINA. Kulikuwa furaha kubwa kwa sababu walikuwepo karibu ASC 20. Zaidi ya Masista wa Divine Providenza na wa Taasisi ya M. De Mattias, walikuwepo masista mbalimbali kutoka Belem, Santarem, Porto de Moz na Manaus kwa ajili ya mkutano wa Nucleus Pará na wa kundi la "Bethany" - ASC wa umri wa kati . Jinsi mkuu wa Region, Sr. Elsie, alivyoongoza tafakari ya kundi la Bethany, sisi sote tulihisi hamu kubwa ya kushiriki katika sikukuu, si tu kwa ajili ya Sr. Serafina lakini pia kwa ajili ya kumbukumbu ya Mt. Gaspar na ya Mashahidi wa Upendo ASC. Katika kushiriki tukio hili hatukupata matatizo safarini, shukrani kwa mchango wa watu marafiki ambao walitusaidia kununua tiketi.

Mpango ulikuwa kama ifuatavyo: katika siku za tarehe 18, 19 na 20 saa 19 kulikuwa na Triduum na tafakari juu ya maisha ya Mtumishi wa Mungu Serafina, Neno la Mungu na maombi kwa ajili ya ASCs na kwa ajili ya watu wengi waliokuwepo.

Tarehe 18: kwenye chuo cha M. De Mattias, kulikuwa na semina yenye mada "Mwanamke aliyewekwa Wakfu".

Tarehe 19: kwenye Kanisa la Bibi yetu wa Msaada wa Daima, kulikwa na semina yenye mada "Mwanamke Misionari".

Tarehe 20: kwenye eneo jipya Mmisionari Padri Frederico, kwenye eneo masikini la pembezoni, kulikuwa na semina yenye mada "Mwanamke Msamaria".

Jumapili tarehe 21, kulikuwa na mlo wa sherehe mchana kwenye bustani ya Nyumba Divina Providenza walikusanyika marafiki na wanafamilia mia mbili ambao walitoa ushirikiano wao kwa kuleta vyakula mbalimbali au vinywaji. Walikuwepo pia Maaskofu.

Muda muhimu zaidi lakini ulikuwa ule wa adhimisho la Ekaristi, aliongoza Askofu Dom João Muniz Alves, Askofu wa Xingu, ambaye aliongea maneno yaliyojaa upendo kuhusu maisha ya Sr. Sarafina. Masista wetu Sr. Jandira, Sr. Zelia na Sr. Clara pamoja na baadhi ya walei waliandaa liturjia nzuri pamoja na alama za maisha ya Mtumishi wa Mungu na Sr. Clara alifundisha kwaya wimbo ulioimbwa ulitungwa na ASC aliyeacha shirika: Utenzi kwa Mtumishi wa Mungu Serafina." Sr. Marilia alitoa muhtasari kuhusu neno la Sr. Maria Paniccia alilokuwa ametuma kwa ajili ya sikukuu, wenye kichwa: NINI ALICHOKUWA ANAONA SERAFINA, akijumuisha maisha ya kishujaa ya Mtumishi wa Mungu. Kwa hayo yote tunamshukuru Mungu.

***Sr. Marília Menezes, ASC***

# Ubunifu

Waabuduo wa Vietnam: Sr. Yen na Sr. Mai na mimi, tulipata fursa ya kutembelea Maasin, jumuiya ASC ya Philippine iliyofunguliwa miaka mitatu tu iliyopota, mahali ambapo Halmashauri ya Foundation inafanya mikutano yake, sisi ambao tuliungana ili kuwepo tu pale, tulibarikiwa kwa kupata ushuhuda ambao walitupa masista wetu wawili, wanaofanya kazi hapa, Sr. Giuliana Gabin na Sr. Ma. Gay Binongo na kuangalia maajabu ambayo utofauti wa upendo wa watu unaweza kufanya.

Katika moja ya nyakati za jioni wakati tulipokuwa pamoja, Sista Flor Manga alikuwa akipiga gitaa na kuimba kwa lugha ya Tagalog jambo zuri. Maneno pekee niliyoweza kuelewa yalikuwa "Maria, Maria, Maria De Mattias". Nilimwomba atafsiri wimbo wake, na muundo wake, alitafsiri wakati huo huo. Niliposema "Ha, tunahitaji kuusikiliza kwa lugha ya kiingereza", yeye alitushirikisha uzoefu wake: "Tunahitaji nyimbo nyingine nyingi kwa lugha ya Tagalog".

Haya ni maneno ya wimbo wake mzuri sana wa sala.

**Maria, Maria, Maria De Mattias**

Damu ambayo ilitiririka kutoka msalabani
Ile inayotoka kwa Yesu
ilijenga ndani ya moyo wako
Hamu ya kumfuata.

Ulitoa maisha yako,
uliyatoa kwa Mungu
Ulimfanya jirani yako asikie
Upendo wa Baba.

Katika ulimwengu wa umasikini
Maumivu na maumivu
Wewe unatufundisha mbinu
Kwa ajili ya kumhudumia jirani.

Upendo wako ni
Msaada wetu na nguvu,
Utuongoze
Kwenye njia sahihi.

Damu azizi ya Yesu
Wokovu wa ulimwengu
Katika msaada na uongozi wako
Isifiwe na wote.



***Sr. Mary Kevin Rooney, ASC***

Eneo la Bara: Ulaya
Region Italia

# Wakati watakatifu wakisonga mbele



Kwenye mkesha wa sikukuu ya watakatifu wote (All Hallows Eve), tarehe 31 Oktoba, chumba cha chakula cha Nyumba Kuu Roma, kilibadilika na kuwa katika karamu ya mbinguni. Hili tukio la mwingiliano wa tamaduni, lililoongozwa na masista wa Amerika ambao wanaishi kwenye Nyumba Kuu, liliiweka jumuiya kwenye jioni ya urafiki na ya furaha pamoja na watakatifu pekee ambao sikukuu ilikuwa inasherehekewa tarehe 1 Novemba. Masista walialikwa kuchagua mtakatifu mmoja muhimu kwa kila mmoja, kuvaa au kushirikisha alama moja na kuandaa habari kwa mtindo wowote (kichekesho, utenzi, masimulizi, n.k). ubunifu ulikuwa wa kutosha uwe katika mavazi ama katika maonyesho (kama inavyoonekana katika picha) na chakula kilituunganisha katika tukio hili la jumuiya na la ushirika. Pipi zilitolea kila baada ya onyesho la mtakatifu.




Watakatifu ambao walitutembelea wakati wa jioni ni: Maria na Giuseppe, Maria De Mattias, Teresa Ua Dogo, Mt. Mattayo mtoza ushuru (alionyeshwa na mhasibu wetu!!!), Oscar Romero, Mt. Alfonsa, Juan Diego, Margherita, Francesco wa Assisi , Mwenye Heri Alojzije Stepinac, Mt. Marta, Mt. Anastasia, Louis/Zelie Martin, Teresa wa Calcutta, Malaika Gabrieli na mama mmoja mtakatifu na Ruthie Longo.

Jioni yetu ilimalizika kwa wimbo na litania ya watakatifu ambao tulishirikishana na kusherehekea maisha yao.

***Sr. Joan Stoverink, ASC***



# Kipindi cha ujana: washa utimilifu wa imani



Mnamo Oktoba 6, 2018, vijana arobaini kutoka nchi nzima ya Poland walishiriki katika mkutano wa vijana huko Warsaw wenye kichwa kipindi cha Ujana. Mkutano ulianza kwa sala ya washiriki wote na kwa kuwasili kwa mabaki ya mwili wa mwenye heri Karolina Kózkówna. Sherehe hii ilikuwa imetanguliwa na maandamano ya watawa masista wakiwa kwenye pikipiki. Hatua muhimu zaidi ya masaa 12 ya ritriti "Kipindi cha ujana: washa ukamilifu wa imani" ilikuwa ni adhimisho la Ekaristi wakishiriki mapadri 600 chini ya uongozi wa Kardinali Kazimierz Nycz, Askofu mkuu wa jimbo kuu la Warsaw.

Askofu Edward Dajczak wa Jimbo la Koszalin-Kołobrzeg, aliwapa mahubiri na kuwauliza washiriki wa mkutano: "Je, mnamjua Yesu?", na aliongeza "Kumjua Yesu kwa kusikia maana yake humjui." Katika mahubiri yake Askofu alisisitiza kuwa maisha ya Kikristo yanajumuishwa katika hamu isiyoisha na katika kumtafuta Yesu daima.

Mkutano kwa ajili ya vijana uliandaliwa kama jibu la hamasa toka upande wa maaskofu kujitolea mwaka huu kwa vijana katika Kanisa na kuishi pamoja nao. Vijana, ambao ni matumaini ya Kanisa na dunia, wakati wa ritriti walipata nafasi ya kusikiliza hotuba na ushuhuda juu ya imani wa watu tofauti: Askofu Mkuu Grzegorz Ryś, Askofu mkuu wa Łódź, wa Martino Zieliński, kiongozi wa jumuiya "Sauti ya Bwana" jamii; Padri Jakub Bartczak, mwandishi wa nyimbo na mtunzi; Bartek Krakowiak, ambaye baada ya uongofu wake aliienda hija kwa miguu kutoka Warsaw hadi Medjugorje; Darek Malejonek, mwanamuziki na mwimbaji; Marcin Jakimowicz, mhariri wa gazeti la kila wiki "Gosc Niedzielny" na mwandishi wa vitabu kuhusu mada za kitawa; Luca Bes, raia na Muniek Staszczyk, mwimbaji wa kundi T. Love.

Washiriki wa ritriti waliweza kuchangia damu au kujiandikisha katika orodha ya wafadhili wa mafuta ya kwenye mifupa, kwenye basi maalum lililoandaliwa, na kwenye uwanja wa Foundation ya Wafadhili ya seli za mirija kwenye mafuta ya mifupa. Vijana waliojaa Roho Mtakatifu na kuimarishwa katika imani kupitia Neno la Mungu, walipata nafasi ya kuungama, kuimba, kucheza na kusali wakimsifu Bwana. Mkutano ulimalizika kwa sala ya pamoja mbele ya Sakramenti Takatifu saa sita usiku.




**Sr. Aldona Kala, ASC**

# "Chukia kosa na si mkosaji"

Binadamu wote wanazaliwa sawa na wanajaliwa haki msingi ambazo hutolewa na Muumba, haki hizi kimsingi ni Haki ya kuishi na uhuru, lakini kama mtu hana heshima na maadili ya jamii, basi mtu huyo hunyimwa haki hizo na kukabiliwa na adhabu.

Nilipotembelea gereza niligundua kwamba wafungwa wengi, wanaume na wanawake, wakiwemo watoto, wanabaki kwenye mahabusu kwa miaka, wakisubiri hukumu ya mahakama. Naamini kuwa lengo kuu la gereza yoyote ni kurekebisha wafungwa ili kuwaunganisha tena na jamii.

Kwa kushirikiana na taasisi za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali tumepanga semina kadhaa kwa lengo la kuleta mageuzi ya mfumo wa sasa magerezani. Mageuzi mengi yanashughulikia utawala wa magereza yenyewe, kama vile swala la kuboresha ubora na wingi wa chakula. Kwa kweli, wafungwa wanadai kwamba kiasi cha fedha zilizotengwa na serikali zitumike kwa mahitaji yao msingi kama vile chai, magazeti, mito na vyakula visivyo vya majani, angalau mara 3 kwa wiki, na kwa ajili ya wanaotumia majani itolewe siagi, jibini na maziwa mtindi, kuheshimu maandalizi na hali ya usafi.



Kwa kuwa urekebishaji wa wafungwa ukishafanyika hupata kazi tu baada ya kutolewa, mpango pia unahusisha kuanzishwa au kufufua vituo vya elimu. Katika magereza mengi, wafungwa wengi, ikiwa ni pamoja na wafungwa wanaume na wanawake maalum, walishiriki katika kozi mbalimbali zilizotolewa na IGNOU (Chuo Kikuu huria cha Indira Gandhi) na vyuo vikuu vya serikali. Kozi zinazotolewa hasa ni BA, (Shahadi katika Sanaa/Bachelor of Arts) MA, (Shahada ya umahiri katika Sanaa/Masters of Arts) MBA (Masters in Business and Adminidtration/ Shahada ya Umahiri katika Utawala na Biashara) na masomo mengine ya elimu ya juu. Wafungwa wachache walishiriki katika madarasa ya elimu ya sekondari ya juu darsa la 10 na la 12 ili kukamilisha elimu yao ya msingi. Kwenye gereza la Bangalore, ili kutoa mafunzo ya ufundi, shule halisi ya kompyuta ilianzishwa.

Wafungwa pia wameanzishiwa kazi za useremala na uchoraji wa vitambaa. Pia ulizinduliwa Mpango kwa ajili ya kuwawezesha wanawake ambapo wanafundishwa kufuma, kutengeneza midoli ya kuchezea, kushona na kudarizi. Mapato yatokanayo na mauzo ya vifaa hivi, aina ya huduma na kazi pia huchangia kuwafanya wajisikie vizuri zaidi kisaikolojia. Semina mbalimbali zinazoandaliwa na mamlaka ya gerezani pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwafanya wafungwa wawe na ujuzi wa haki zao za kisheria, masuala ya afya na usafi, VVU / UKIMWI, matatizo ya afya ya akili, watoto wadogo na hatua za kupunguza vurugu katika magereza.

Mfumo wa magereza wa sasa ni wa kisasa na wenye ufanisi zaidi kwa mundo wa kifungo. Kumekuwa na hatua kadhaa zilizochukuliwa ili kuboresha hali katika magereza, lakini bado mengi yanapaswa kufanyika. Serikali ya Jimbo la Karnataka, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali na utawala wa magerezan, inafanya kazi kwa undani katika mipango hii ya kuboresha magereza.

Haya mageuzi na mazoezi yaliyofanyika kwenye magereza ili kubadili mtazamo wa jadi na wa kikoloni wa mfumo wa magereza ya India yamekuwa chanzo cha msukumo kwangu kwa sababu huwasaidia wafungwa kuwa watu wenye ubunifu zaidi na wananchi wanaowajibika zaidi.

***Sr. Shainy Kayyaniyil, ASC***

## Kalenda ya Uongozi Mkuu




**1 Disemba:** Sr. Nadia Coppa na Sr. Matija Pavić watakuwa Bari kwa ajili baraka ya mchoro wa picha ya Mt. Maria De Mattias Parokia ya Damu Azizi.
**3-23 Disemba:** Sr. Nadia Coppa, Sr. Manuela Nocco, na Sr. Bridget Pulickakunnel watakuwa kwenye ziara Tanzania
**15 Disemba:** Siku ya ritriti kwa ajili ya maandalizi ya Noeli
**22 Disemba:** Chakula cha jioni ya Noeli pamoja na ASC waliomo kwenye eneo
**27 Disemba:** Mchezo waTombola, muunganiko wa mashirika

## Sikukuu za Kuzaliwa: tunasherehekea maisha



| | | |
|---|---|---|
| miaka 40 | | |
| **Sr. Yulita Mkafuraha Gabriel Kitutu** | 01/12/1978 | Tanzania |
| **Sr. Maria Magdalena Michael Stephan** | 10/12/1978 | Tanzania |
| miaka 80 | | |
| **Sr. Maria D'Avila Martins Guimarães** | 09/12/ 1938 | Manaus |
| **Sr. Wirginia Czerepak** | 10/12/1938 | Wrocław |
| **Sr. Jean Marie Kumke** | 14/12/1938 | USA |
| **Sr. Concetta Maselli** | 07/12/1938 | Italia |
| **Sr. Olga Petruzzelli** | 21/12/1938 | Italia |
| **Sr. Giulia Forese** | 24/12/1938 | Italia |
| miaka 90 | | |
| **Sr. Leonarda Bardella** | 20/12/1928 | Italia |



## Waliorudi Nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 11/11/2018 | **Sr. Marta Carvalho dos Santos** | Manaus |
| 23/11/2018 | **Sr. Maria Righi** | Italia |
| 3/12/2018 | **Sr. Rossana Mazzocchini** | Italia |


Gazeti la Kimataifa
Waabuduo Damu ya Kristo
...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**

*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 13, Disemba 2018**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin*** *- Kijerumani*